


# RUZUKU YA KUKUZA UFIKIAJI, HAKI, NA USAWA (FARE)

## RUZUKU YA FARE NI NINI?

Idara ya Leba ya Jimbo la New York (NYS DOL) ilipokea ruzuku kutoka kwa Ofisi ya Wanawake ya Idara ya Leba ya Marekani ili kufanya uhamasishaji na mawasilisho kwa wanawake yanayolenga haki na manufaa za ajira. Tunalenga kufikia wanawake waliotengwa na wasio na uwakilishi wa kutosha nje ya Jiji la New York, hasa katika maeneo ya mashambani, kupitia mawasilisho na hafla za ana kwa ana na za mtandaoni. Lengo letu ni kueneza elimu na maarifa ili kuwawezesha wanawake katika jimbo lote, kwa kufanya hivyo, tutawasaidia wanawake kupewa kipaumbele katika kupokea haki na manufaa katika jamii zao.

## JE, NINAWEZAJE KUTUMA OMBI LA KUPATA WASILISHO?

Wasiliana na NYSDOL kwa barua pepe kwa **info.nysdol@labor.ny.gov** au upige simu kwa **888-4-NYSDOL (888-469-7365)**.

## MADA ZINAZOLENGWA

### KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA

Wafanyakazi wote wa Jimbo la New York (NYS) wana haki ya kupokea angalau kima cha chini cha mshahara kwa saa.

| ENEO | KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA *kuanzia tarehe 1/1/2024* | |
|---|---|---|
| Jiji la New York, Long Island na Kaunti ya Westchester | dola 16.00/saa | dola 18.55/saa Wasaidizi wa Huduma ya Nyumbani |
| Sehemu zingine za Jimbo la New York | dola 15.00/saa | dola 17.55/saa Wasaidizi wa Huduma ya Nyumbani |

### KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA KWA WAFANYAKAZI WANAOPOKEA BAHASHISHI

Sheria ya NYS inaruhusu waajiri katika sekta nyingi kuzingatia kima cha chini cha mshahara kwa kuchanganya mshahara unaolipwa na mwajiri na bahashishi ambazo mfanyakazi hupokea kutoka kwa wateja. Waajiri wa tasnia ya utoaji wa huduma kama vile hoteli na utalii pekee ndio wanaoruhusiwa kuchukua pesa za kiwango sawa na bahashishi kutoka kwa mshahara wa chini. Kazi zinazolipwa kwa bahashishi pekee haziruhusiwi.

| ENEO | WAFANYAKAZI WA HUDUMA *kuanzia tarehe 1/1/2024* | WAFANYAKAZI WA HUDUMA YA CHAKULA *kuanzia tarehe 1/1/2024* |
|---|---|---|
| Jiji la New York, Long Island na Kaunti ya Westchester | Mshahara wa dola 13.35 Pesa za Bahasishi dola 2.65 | Mshahara wa dola 10.65 Pesa za Bahasishi dola 5.35 |
| Sehemu zingine za Jimbo la New York | Mshahara wa dola 12.50 Pesa za Bahasishi dola 2.50 | Mshahara wa dola 10.00 Pesa za Bahasishi dola 5.00 |

### SAA ZA ZIADA ZA KAZI

Wafanyakazi wengi wanapaswa kupokea malipo ya saa za ziada za kazi baada ya kufanya kazi kwa saa 40 katika wiki ya kazi. Malipo ya saa za ziada za kazi ni mara 1½ ya malipo yako ya kawaida. Kwa wafanyakazi wanaopewa bahashishi, waajiri lazima walipe malipo ya saa za ziada za kazi kwa mara 1½ ya kima cha chini cha mshahara, kisha kuondoa kiwango kinachotumika cha pesa alizopata kutoka kwa bahashishi. Wafanyakazi wa kilimo kwa sasa hupata malipo ya saa za ziada baada ya kufanya kazi kwa saa 56 katika wiki ya kazi na kwa saa zozote walizofanya kazi katika siku iliyoteuliwa apumzike.

### UAINISHAJI MBAYA: MFANYAKAZI ALIYEAJIRIWA AU MFANYAKAZI HURU?

Ili kubaini ikiwa mfanyakazi anafaa kuainishwa kama mfanyakazi aliyeajiriwa au mfanyakazi huru, hali ya uhusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa lazima izingatiwe. Wafanyakazi huru wanafanya biashara yao wenyewe na wanatoa huduma zao kwa umma kwa ujumla.

Mfanyakazi huru hufanya kazi yake bila ya:

- Usimamizi
- Maelekezo
- Udhibiti

Kwa upande mwingine, uhusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa unaweza kuwepo ikiwa mwajiri:

- Anachagua lini, wapi na jinsi mfanyakazi atatoa huduma
- Anatoa mahali pa kufanyia kazi, vifaa, zana na bidhaa
- Anasimamia kazi moja kwa moja
- Huweka saa za kazi na kiwango cha malipo, nk.

Jifunze zaidi hapa: **dol.ny.gov/independent-contractors**

Mwajiri anapoainisha vibaya mfanyakazi kimakusudi kama mfanyakazi huru, huo ni ulaghai. Baadhi ya waajiri hutumia mbinu hii ili kuepuka kufuata sheria ya Bima ya Watu Wasio na Ajira, Fidia ya Wafanyakazi, Usalama wa Kijamii, ulipaji wa kodi na kima cha chini cha mshahara. Ripoti ulaghai kwa NYS DOL mtandaoni kwa **dol.ny.gov/report-fraud** au upige simu kwa nambari maalum ya simu ya saa 24: **866-435-1499**.

# JUA HAKI ZAKO KAMA MFANYAKAZI MWANAMKE KATIKA NYS

## SHERIA YA KUWEKA WAZI UNACHOLIPWA

Kuanzia Septemba 17, 2023, waajiri wa NYS walio na wafanyakazi wanne (4) au zaidi sharti wajumuishe kiwango cha mshahara au safu ya mishahara katika matangazo yao ya kazi kwa kazi zote zinazopaswa kufanywa, angalau kwa sehemu, katika jimbo la New York. Matangazo ya kazi sharti yatangaze kiwango cha malipo au safu ya malipo ambayo mwajiri anaamini, kwa nia njema, kuwa ya kweli wakati wa kutangaza na inapaswa kumpa mtuma ombi mtarajiwa wazo halali la anachotarajia kulipa.

## SHERIA YA KUPIGA MARUFUKU MWAJIRI KUULIZA HISTORIA YA MSHAHARA YA MWAJIRIWA

Kuanzia Januari 6, 2020, waajiri wa NYS hawataweza tena kuwauliza watuma maombi ya kazi kuhusu historia ya mshahara na manufaa yao, na maelezo haya hayawezi kutumika kama kipengele cha kuamua iwapo watamhoji au kumpa ajira mtuma ombi. Malipo unayotarajiwa kulipwa yanaweza kujadiliwa, na watu binafsi wanaweza kuchagua kufichua historia ya mishahara yao kwa madhumuni ya mazungumzo.

## NOTISI ZA MALIPO

Unapoajiriwa, mwajiri wako lazima akupe notisi ya malipo ambayo ina maelezo fulani muhimu, kama vile:

- Kiasi na mara utakazolipwa
- Siku ya kawaida ya malipo, na
- Makato yoyote kutoka kwa malipo yako

## USAWA WA MALIPO

Ni kinyume cha sheria kwa mwajiri kumlipa mwanamke kiasi kilicho chini ya mwanamume kwa kufanya kazi sawa kwa misingi tu ya jinsia. Tofauti za malipo zinaweza kutegemea cheo, kazi nzuri, au kipengele cha ukweli kisichokuwa jinsia, kama vile elimu au uzoefu.

## KARATASI YENYE MAELEZO YA MALIPO NA MAKATO

Lazima ulipwe kwa saa zote ulizofanya kazi. Unaweza kulipwa kwa pesa taslimu au hundi, lakini lazima upewe karatasi yenye maelezo ya kina ya malipo kila unapolipwa.

Mwajiri hawezi kukutoza kwa kuvunjika kwa kifaa, kuharibika, uharibifu, gharama za sare na matengenezo, gharama za kufanya biashara za mwajiri, au uhaba wa pesa taslimu.

## UFIKIAJI WA LUGHA

Mashirika ya NYS ambayo hutoa huduma za umma za moja kwa moja yanahitajika kutoa huduma za ukalimani na tafsiri za fomu na maagizo muhimu kwa umma bila malipo. Huduma za ukalimani wa lugha zinatolewa katika zaidi ya lugha 200, ikiwa ni pamoja na lugha ya ishara. Katika NYS DOL, hati muhimu zilizoandikwa hutafsiriwa katika lugha 16 kuu za serikali ya jimbo.

## KUKAMA MAZIWA YA MAMA KATIKA MAHALI PA KAZI

Kwa hadi miaka mitatu (3) baada ya kujifungua, kina mama wanaonyonyesha wana haki ya kuchukua muda wa mapumziko usio na malipo au kutumia muda wa mapumziko unaolipwa au muda wa kula chakula kila siku, kukama maziwa ya mama kazini. Waajiri wote wa NYS wanahitajika kutenga eneo la faragha la kukamia karibu na eneo la kazi la mwajiri ambalo linaweza kuwa kiti, meza au sehemu nyingine tambarare, taa, sehemu ya umeme (ikiwa mahali pa kazi pana umeme), na ufikiaji wa karibu wa maji safi, yanayotiririka.. Sehemu hii haiwezi kuwa msala.

## UNYANYASAJI WA KINGONO KAZINI

Waajiri wote katika NYS wanapaswa kudumisha mazingira ya kazini yasiyo na unyanyasaji wa kingono. Kisheria, waajiri sharti wawe na sera ya kuzuia unyanyasaji wa kingono na watoe nakala kwa wafanyakazi wote pamoja na mafunzo ya kila mwaka.

## LIKIZO INAYOLIPWA YA KUUGUA NA USALAMA

Wafanyakazi wa sekta ya kibinafsi katika NYS wanalindwa chini ya sheria ya Likizo Inayolipwa ya Kuugua na Usalama. Kwa kiwango cha chini zaidi, wafanyakazi hupata saa moja (1) ya likizo ya kuugua na usalama kwa kila saa 30 wanazofanya kazi. Suala la ikiwa likizo inalipwa au hailipwi inategemea uwezo wa mwajiri.

## BIMA YA WATU WASIO NA AJIRA

Ikiwa ulifanya kazi katika NYS na ukapoteza kazi yako bila kosa lako mwenyewe, unaweza kustahiki Bima ya Watu Wasio na Ajira. Lazima uwe na mapato ya kutosha ili kuweka ombi la malipo; uwe tayari, uwe unakubali, na uwezo wa kufanya kazi; ukiendelea kutafuta kazi; na kurekodi juhudi zako za utafutaji wa kazi. Tuma ombi mtandaoni kwa **dol.ny.gov** au piga simu kwa **888-209-8124**.

## JE, NITAWASILISHAJE MALALAMIKO?

Ugavi wa Viwango vya Kazi husaidia kutatua ukiukaji wa sheria ya kazi ya NYS. Ni kinyume cha sheria kwa mwajiri kumfuta kazi, kumwadhibu, au kumbagua au kulipiza kisasi kwa mfanyakazi kwa namna yoyote kwa kuwasilisha malalamiko kuhusu uwezekano wa ukiukaji wa sheria ya kazi au kutekeleza haki zozote zinazolindwa chini ya sheria ya kazi ya NYS.

Wasilisha fomu ya **LS223** ili kuwasilisha malalamiko. Wasiliana na Ofisi ya Viwango vya Kazi kwa maelezo zaidi: **888-52-LABOR (888-525-2267)** au **LSAsk@labor.ny.gov**.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea **dol.ny.gov/fostering-access-rights-and-equity-fare-grant**

Idara ya Leba ya Jimbo la New York ni Mwajiri/Mpango Unaotoa Fursa Sawa.
Vifaa na huduma za usaidizi zinapatikana vikiombwa na bila malipo kwa watu wenye ulemavu TTY/TDD 711 au 1-800-662-1220 (Kiingereza) / 1-877-662-4886.
Ruzuku ya FARE inafadhiliwa na ruzuku ya serikali kuu ya dola 350,000, ambayo ni asilimia 100 ya bajeti yake. Asilimia 0, au dola 0 inafadhiliwa na vyanzo vya serikali au visivyo vya kiserikali.